

Mradi Na. 4283: UJENZI WA MKONGO WA TAIFA WA MAWASILIANO

Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 **Sh. 149,700,000,000** ziliidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 149,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 700,000,000** ni fedha za nje. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Kufanya Ujenzi wa Mkongo wa Majini kiasi cha Kilomita 60 kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika;
- (ii) Kufanya tathmini ya Ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi Data Zanzibar;
- (iii) Kuwajengea uwezo wataalam 150 kwenye TEHAMA;
- (iv) Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;
- (v) Kukamilisha Nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sheria ya TEHAMA na Mkataba wa Jumuiya ya Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Malabo Convention);
- (vi) Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni;
- (vii) Kuwezesha utendaji kazi wa Kamati za Kiufundi kwa ajili ya usimamizi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;
- (viii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa mradi; na
- (ix) Kuandaa Mpango Mkuu (Master Plan) wa utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Hadi kufikia tarehe **12 Januari, 2023** Wizara ilipokea jumla ya **Sh. 39,600,496,772.18** sawa na asilimia **26.5** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

- (i) Ununuzi wa mitambo kwa ajili ya vituo 111 vya kutolea Huduma (transmission and power equipments) umekamilika ambapo usimikaji umefanyika kwenye vituo 26 vya kutolea huduma (Point of Presence-POPs and Optical Line Amplifiers OLA) kwenye maeneo ya Dar es Salaam, Chalinze Tanesco, Chalinze TTCL, Manga, Hale Tanesco, Hale TTCL, Tanga, Horohoro, Mkomazi, Same, Mwanga, Moshi, Arusha, Makuyuni, Babati, Namanga, Morogoro, Kidatu, Ifakara, Kihansi, Iringa, Mtera, Dodoma, Manyoni, Singida na Katesh. Usimikaji katika vituo vingine 85 utakamilika mwezi Juni, 2023 baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mkongo wa Mawasiliano na majengo ya vyumba vya mitambo;

- (ii) Marekebisho ya vyumba vya mitambo 39 vya mkongo wa Taifa (Civil Works) umefanyika kwenye maeneo ya Bariadi, Tukuyu, Miangalua, Kizi, Uvinza, Kibondo, Kabanga, Rusumo, Mutukula, Mabuki, Nassa, Ikwiriri, Mikumi, Kidatu, Ifakara, Njombe, Makambako, Mafinga, Iringa, Hulia, Tunduru, Michiga, Masasi, Tandahimba, Lindi, Mitole, Somanga, Kimanzichana, Chalinze, Bagamoyo, Chunya, Horohoro, Igunga, Kahama, Kilosa, Manga, Nzega, Namanga na Chimala.
- (iii) Nguzo (OFC Poles and Accessories) 4,775 zimesimikwa kati ya nguzo 19,915 zitakazotumika kujenga mkongo wa juu (Overhead Fiber Installation) kwenye maeneo mbalimbali ya njia za Mkongo. Nguzo hizi pia zitatumika na TANESCO kwa ajili ya kupitisha umeme kwenye maeneo ambayo hayana umeme;
- (iv) Ukamilishaji wa Ujenzi wa njia mpya za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umefanyika zenye jumla ya Kilometa 1,663 kati ya Kilometa 4,442 zilizokuwa zimepangwa kujengwa;
- (v) Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA Desktops-184, Kompyuta mpakato-210, Scanners-50 na *TTCL modems* 200 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa 'case management' kwa ajili ya kurekodi matukio ya uhalifu wa mtandao;
- (vi) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa jumla ya vijiji 2,116 visivyokuwa na mawasiliano. Taarifa ya upembuzi yakinifu itatumika kuandaa andiko dhana la mradi kwa ajili ya kuomba fedha katika Benki ya Exim ya China ili kufanya ujenzi wa minara kwenye vijiji hivyo.
- (vii) Kukamilika kwa utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Data Protection Act,2022) iliyosainiwa Novemba, 2022 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali tarehe 2 Disemba,2022;